**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

**Toleo Na: 1444 H / 031** | **Ijumaa, 18 Sha'aban 1444 H** | **10/03/2023 M**

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## Uzinduzi wa Tovuti ya Kifaransa ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir (Imetafsiriwa)

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir inafuraha kutangaza kuzinduliwa kwa tovuti yake kwa lugha ya Kifaransa, ambayo itatumika kama tovuti ya watu wanaozungumza Kifaransa kutazama maudhui ya habari yanayoangazia juhudi zilizofanywa katika mradi wa kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume.

Uzinduzi huu wenye baraka Insha'Allah ni matunda ya juhudi zisizokoma zinazofanywa na Hizb ut Tahrir na wanachama wake kuongeza mawasiliano na watu ili kuwafikia watu/ wafuasi wengi wa Ummah wa Kiislamu kadiri inavyowezekana, popote walipo.

Mradi wa kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume unasonga mbele kwa uthabiti na ukali zaidi.

Kuanguka kwa Khilafah na fahari iliyokuwa nayo kwa Ummah mzima wa Kiislamu kunaombolezwa, huku umuhimu wa kuuelewa vyema Uislamu na mfumo wake wa utawala unazidi kuwa na hamu miongoni mwa vijana wa Ummah.

Hapa inakuja dori ya taswira ya vyombo vya habari, ambayo inafikisha ujumbe wa Uislamu kama kadhia nyeti, lazima ipate ufahamu wa kufahamu mambo mahsusi ya mfumo wa Kiislamu, nini maana ya kusimamisha tena Khilafah, na jinsi njia ya Utume inavyotumika kuisimamisha na kuitawala.

Kwa sababu hii, tunawataka wanahabari wote wa kweli katika harakati zao za kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume, hususan wanahabari wanaozungumza Kifaransa, kuhakiki nyenzo zilizowekwa kwenye tovuti ya lugha ya Kifaransa ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir. Tukimuomba Mwenyezi Mungu awape ilham bora ya mambo yao na avue kutokana nayo yale yanayokamilisha kazi kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah.

Tunazindua tovuti ya lugha ya Kifaransa ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir kwa baraka za Mwenyezi Mungu na tunamuomba atuongoze kwa kile Anachokipenda na anachofurahishwa nacho.

Mwenyezi Mungu (swt) asema,

(وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيداً عَلَيْهِم مِّنْ أَنفُسِهِمْ وَجِئْنَا بِكَ شَهِيداً عَلَى هَؤُلاء وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَاناً لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ)

**"Na (waonye) siku tutakapo wainua mashahidi katika kila umma wakiwashuhudia kwa yanayo tokana na wao, na tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hao. Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu,na rehema, na bishara kwa Waislamu."** [An-Nahl: 89].

Link ya Tovuti: https://www.hizb-ut-tahrir.info/fr/

**Mhandisi Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Simu\Kipepesi:** 009611307594 **Rununu:** 0096171724043

**Pepe:** media@hizb-ut-tahrir.info

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti Rasmi ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
www.hizb-ut-tahrir.info